



TAMKO KULAANI KUKAMATWA KWA WAANDISHI WA HABARI KANDA YA ZIWA

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) unalaani vikali vitendo vya kukamatwa kwa waandishi wa habari mbalimbali nchini hasa siku za hivi karibuni. Usiku wa kuamkia leo Juni 18, 2024 mwandishi wa habari Constatine Mathias wa Uhuru Media mkoani Simiyu amekamtwa. Polisi walikagua nyumbani kwake na wakachukua vifaa vyake vya kazi ikiwemo simu la laptop yake.

Hadi kufikia muda huu bado Polisi hawajaweka wazi ni wapi wanamshikilia mwandishi huyo na tuhuma zipi zinamkabili ingawa inasemekana amesafirishwa kupelekwa mkoani Mwanza.

Vilevile, mnamo Juni 13, 2024 mwandishi wa habari na mmiliki wa Dima Online Tv, Dinna Maningo, alikamatwa nyumbani kwake Tarime mkoani Mara na kusafirishwa hadi mkoani Mwanza kwa tuhuma za kutumia nyaraka za siri za Jeshi la Polisi za kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Yahaya Nawanda, anayedaiwa kumlawiti binti wa miaka 21 mnamo Juni 2, 2024 usiku katika eneo la baa ya the Cask, viwanja vya jengo la Rock City Mall.

Hadi leo hii mwandishi huyo bado anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza bila ya kupewa dhamana kinyume cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

Tarehe 16 Juni 2024 Mwandishi wa habari ambaye pia ni Naibu Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Jamhuri, Manyerere Jackton, alikamatwa na kushikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro, kwa zaidi ya saa mbili na nusu kwa tuhuma za kupiga picha lori lililopinduka. Akiwa safarini eneo la mji wa Same, Manyerere alikuta lori lililobeba mafuta ya kula likiwa limepinduka na wananchi wanaokadiriwa kuwa hadi 200 wamelivamia wakiwa na ndoo na madumu yaliyoashiria kuchota mafuta hayo.

Bw. Manyerere baada ya kukuta tukio hilo saa 4:00 asubuhi alipiga picha na akiwa katika kufanya hivyo, ghafla Polisi wasiozidi saba walimvamia na kuanza kumghasi kisha kuchukua simu aliyokuwa akiitumia kupiga picha na kufuta kila alichorekodi.

Baada ya kukamatwa, Bw. Manyerere alipelekwa kituo Kikuu cha Polisi Wilaya ya Same, kwa lengo la kumhoji lakini aliachiwa baadaye kwa amri ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Simon Maigwa.

Kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 waandishi wa habari wana haki na uhuru wa kukusanya taarifa ikiwa ni pamoja na kuuhabarisha umma juu ya taarifa hizo, hivyo kwa namna yoyote ile ni makosa na ni kinyume cha Katiba na Sheria za nchi kuwakamata waandishi wa habari wakiwa wanatekeleza majukumu yao.

Hatua ambazo Mtandao Umeshachukua

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania ulitoa maelekezo kwa wakili Amri Linus aliyepo mkoani Mwanza kushughulikia kesi za waandishi wote wawili waliokamatwa mkoani Mwanza. Hata hivyo, dhamana haijaweza kupatikana kwa mwandishi Maningo hivyo asubuhi ya leo wakili Linus ameshafungua kesi Mahakama Kuu masijala ya Mwanza dhidi ya Jeshi la Polisi mkoni Mwanza ili kudai dhamana ya mwandishi Maningo.

Wito wetu

- Mtandao unatoa wito kwa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kuwaachia mara moja mwandishi wa habari Dina Maningo na Constatine Mathias kwani hawani watoa taarifa tu ambazo Polisi wanapaswa kuzifanyia kazi na sio kuwakamata na kuwakweka kizuizini kinyume cha Sheria.
- Mtandao unatoa wito kwa Jeshi la Polisi mkoani Mwanza kuwarudishia waandishi wa habari vifaa vyao vya kufanyia kazi ili kuhakikisha kwamba wasiingie gharama ya kununua vifaa vingine. Hii itawasaidia waandishi hao pia kuendelea kufanya kazi ya kuipasha habari jamii ambayo ndio kazi mama ya mwandishi wa habari.
- Mtandao unatoa wito kwa Jeshi la Polisi kufanya upelelezi kwa kuzingatia Sheria na Amri Kuu za Jeshi la Polisi (PGO) ili kuhakikisha kwamba haki za waandishi wa habari hazikiukwi kwa makusudi.

Imetolewa na,

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC),

Juni 18, 2024

Dar es Salaam, Tanzania.